

**JUMUIYA YA UFUNDISHAJI WA MASOMO YA KIISLAMU TANZANIA (TISTA)**  
**FOMATI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**  
**R10 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

### **1.0 UTANGULIZI**

Fomati hii inatokana na muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu wa mwaka 2012 na itaanza kutumika mwaka 2026. Fomati hii imejikita katika kupima kiwango cha ujifunzaji wa wanafunzi wa Darasa la Kwanza, la Pili, la Tatu na Darasa la Nne katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

Upimaji huu una lengo la kumjengea mwanafunzi udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake. Upimaji wa somo hili utakuwa na maswali **sita (6)** yenye jumla ya vipengele **35**.

### **2.0 MALENGO YA JUMLA**

Upimaji wa Elimu ya Dini ya Kiislamu unalenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

- 2.1 Kusoma na kuhifadhi juzuu ya 30 katika Qur'an kwa kufuata hukumu na kueleza mafunzo yake;
- 2.2 Kufafanua nguzo za Imani ya Kiislamu;
- 2.3 Kufafanua Nguzo za Uislamu;
- 2.4 Kutekeleza ibada mbalimbali ipasavyo;
- 2.5 Kutofautisha baina ya sunnah na Hadith;
- 2.6 Kubainisha matendo na mwenendo unaoonesha tabia njema ya Kiislamu;
- 2.7 Kueleza historia ya Uislamu kabla na wakati Mtume Muhammad (S.A.W) akiwa Makka na Madinah

### **3.0 UJUZI WA JUMLA**

Upimaji wa Elimu ya Dini ya Kiislamu unalenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

- 3.1 Kusoma na kuhifadhi juzuu ya 30 katika Qur'an kwa kufuata hukumu na kueleza mafunzo yake;
- 3.2 Kufafanua nguzo za Imani ya Kiislamu;
- 3.3 Kufafanua Nguzo za Uislamu;
- 3.4 Kutekeleza ibada mbalimbali ipasavyo;
- 3.5 Kutofautisha baina ya sunnah na Hadith;
- 3.6 Kubainisha matendo na mwenendo unaoonesha tabia njema ya Kiislamu;
- 3.7 Kueleza historia ya Uislamu kabla na wakati Mtume Muhammad (S.A.W) akiwa Makka na Madinah

### **4.0 MUUNDO WA MTIHANI**

Upimaji wa Elimu ya Dini ya Kiislamu utakuwa na karatasi **moja (1)** na utafanyika kwa muda wa **saa 1:30** kwa watahiniwa wote isipokuwa kwa watahiniwa wenye mahitaji maalum ambapo mtihani wao utafanyika kwa **saa 1:45**. Upimaji utakuwa na sehemu A na B zenye jumla ya maswali **sita (6)** yenye jumla ya vipengele **35**. Mtihiniwa atatakiwa kujibu maswali yote. Jumla ya alama zitakuwa **50**.

**Sehemu A** itakuwa na maswali **matatu (3)**; swali la kwanza, la pili na la tatu yenye jumla ya vipengele **20**. Swali la kwanza litakuwa na vipengele **10** vya maswali ya kuchagua herufi ya jibu sahihi kati ya machaguo matano (**A-E**) aliyopewa kuhusu **Tarekh**. Swali la pili litakuwa na vipengele **vitano (5)** vya kuoanisha kutoka katika fani ya **Fiqh**. Swali la tatu litakuwa la

kuchagua jibu sahihi katika mabano/kisanduku na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi na litakuwa na vipengele **vitano (5)** kuhusu Akhlaq/Sunnah na Hadith. Kila kipengele katika swali la kwanza hadi la tatu kitakuwa na alama **moja (1)**, hivyo, sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **20**.

**Sehemu B** itakuwa na maswali **matatu (3)** ya majibu mafupi yenye jumla ya vipengele **15**. Swali la nne litakuwa la kujaza nafasi zilizoachwa wazi au la kupanga dhana katika mtiririko wenye kuleta mantiki, litahusu fani ya Qur'an na litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Swali la tano litahusu fani ya Tawhiid na litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Swali la sita litahusu fani ya Fiqh na litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Kila kipengele katika swali la nne hadi la sita kitakuwa na alama **mbili (2)**, hivyo, sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **30**.

## 5.0 FANI/MADA ZITAKAZOTAHINIWA

Watahiniwa watapimwa katika fani/mada zifuatazo:

- 5.1 Qur'an
- 5.2 Tawhiid
- 5.3 Fiqh
- 5.4 Akhlaq
- 5.5 Sunnah na Hadith
- 5.6 Tarekh

## 6.0 Jedwali la Utahini: R10 Elimu ya Dini ya Kiislamu

Na	Fani/Mada	Viwango Vya Umahiri Vitakavyopimwa						Idadi ya Vipengele vya Maswali kwa kila Fani/mada	Asilimia ya uzito kwa kila fani/Mada
		Kukumbuka	Kuelewa	Kutumia	Kuchambua	Kutathimini	Kuunda		
1	Fiqh							10	28.6
2	Tarekh							10	28.6
3	Tawhiid							5	14.3
4	Qur'an							5	14.3
5	Akhlaq/Sunnah na Hadith							5	14.3
<b>Jumla</b>								<b>35</b>	<b>100</b>